



TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA  
Kitalu Na. 8, Mtaa wa Luthuli  
S.L.P 2643, DAR ES SALAAM  
Simu: +255 22 2135747/8; 2137125; 2135222  
Faksi: +255 22 2111281  
Barua Pepe: [chragg@chragg.go.tz](mailto:chragg@chragg.go.tz)  
Tovuti: [www.chragg.go.tz](http://www.chragg.go.tz)

Oktoba 27, 2015

## **TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

### **Tamko la Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kukemea vurugu na uvunjifu wa taratibu na sheria**

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za vurugu zinazotokea katika maeneo mbalimbali nchini wakati huu wa kusubiri kutangazwa rasmi kwa matokeo ya uchaguzi wa Rais. Wabunge na Madiwani uliofanyika Oktoba 25, 2015.

Aidha, Tume imesikitishwa na hatua ya baadhi ya wanasiasa kuingilia majukumu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), ikiwa ni pamoja na kujitangazia matokeo ya uchaguzi kinyume cha taratibu na sheria za uchaguzi.

Tume inapenda kuchukua fursa hii kukemea vitendo hivyo vinavyofanywa na wanasiasa na wafuasi wao ambavyo siyo tu vinaashiria uvunjifu wa sheria, taratibu na kanuni za uchaguzi ambao unaweza kusababisha uvunjifu wa amani na utulivu, haki za binadamu na vitendo vinavyokwenda kinyume na misingi ya utawala bora.

Kwa taarifa tulizonazo vurugu hizo zinazotokea katika maeneo machache ya Tanzania Bara na Zanzibar zimelilazimu Jeshi la Polisi kutumia nguvu, ili kuhakikisha kuwa utulivu na amani ambao tumeushuhudia unaendelea.

Kwa kuwa nchi yetu inaongozwa na utawala wa sheria, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inawataka wadau wote wa uchaguzi waongozwe na sheria za nchi.

Kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi, zinazosimamiwa na NEC na ZEC Tume za Uchaguzi ndizo zenye mamlaka ya kutangaza matokeo ya uchaguzi.

Ili Taifa letu liendeleo kuwa na utulivu katika kipindi hiki cha kusubiria kutangazwa rasmi kwa matokeo ya uchaguzi Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora:

1. Inawataka wadau wote wa uchaguzi wakiwemo viongozi wa vyama vya siasa, wagombea, watendaji wa mamlaka za uchaguzi, na Serikali kuheshimu sheria za uchaguzi na kila mmoja kutimiza wajibu wake.
2. Tume (THBUB) inawakumbusha Wagombea wasijitangazie matokeo yao wenyewe ili kuepuka uvunjifu wa sheria na mkanganyiko unaoweza kusababisha vurugu na uvunjifu wa amani.
3. Aidha, THBUB inawataka wanasiasa na wananchi kwa ujumla wawe watulivu na wasiziingilie kazi za NEC na ZEC.
4. Inawasihi wanasiasa, wagombea na wananchi kwa ujumla wawe watulivu katika kipindi hiki cha kusubiri matokeo rasmi na wajiepushe na vitendo vinavyoashiria uvunjifu wa amani na haki za binadamu. Kama kuna malalamiko yoyote, sheria na taratibu stahiki zifuatwe

Tume inawataka wananchi watakaobaini uvunjifu wowote wa haki za binadamu, au uvunjifu wa sheria ya uchaguzi, kuzijulisha mamlaka husika zinazosimamia zoezi la uchaguzi. Aidha, wanaweza kutoa taarifa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kupitia ujumbe mfupi wa simu ya kiganjani (SMS) kwenda Na. **0754 460 259**.

Ujumbe lazima uanze na neno 'TAARIFA' au ' RIPOTI' kisha andika taarifa yenyewe. Namba hii inapokea ujumbe mfupi tu. Kwa taarifa zaidi piga Na. **+255 22 2135747- 8**.

Imetolewa na:

  
Bahame Tom Nyanduga  
**Makamu Mwenyekiti**

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Oktoba 27, 2015